Yuda

Salamu

1 Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo na nduguye Yakobo:
Kwa wale walioitwa, wapendwa katika Mungu Baba na kuhifadhiwa salama ndani ya Yesu Kristo:
2 Rehema, amani na upendo viwe kwenu kwa wingi.

Dhambi Na Hukumu Ya Watu Wasiomcha Mungu

3 Wapendwa, ingawa nilikuwa ninatamani sana kuwaandikia kuhusu wokovu ambao tunaushiriki sisi sote, niliona imenipasa kuwaandikia na kuwasihi kwamba mwitetee imani iliyokabidhiwa watakatifu kwa nafasi moja itoshayo.
4 Kwa kuwa kuna watu waliojipenyeza kwa siri katikati yenu, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, waovu, wapotoshao neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi wakimkana yeye aliye Bwana wetu wa pekee, Bwana Yesu Kristo.

Hukumu Kwa Walimu Wa Uongo

5 Ingawa mmekwisha kujua haya yote, nataka niwakumbushe kuwa Bwana akiisha kuwaokoa watu wake kutoka nchi ya Misri, baadaye aliwaangamiza wale ambao hawakuamini.
6 Nao malaika ambao hawakulinda nafasi zao, lakini wakayaacha makao yao, hawa amewaweka katika giza, wakiwa wamefungwa kwa

minyororo ya milele kwa ajili ya hukumu Siku
ile kuu.
7 Vivyo hivyo, Sodoma na Gomora na pia ile
miji iliyokuwa kandokando, ambayo kwa jinsi
moja na hao, walijifurahisha kwa uasherati na
kufuata tamaa za mwili zisizo za asili, wali-
wekwa wawe mfano kwa kuadhibiwa katika
moto wa milele.

8 Vivyo hivyo, hawa waotao ndoto huutia
mwili unajisi, hukataa kuwa chini ya mamlaka
na kunena mabaya juu ya wenye mamlaka.

9 Lakini hata malaika mkuu Mikaeli alipokuwa
anashindana na ibilisi juu ya mwili wa Mose,
hakuthubutu kumlaumu, bali alimwambia,
“Bwana na akukemee!”
10 Lakini watu hawa hunena mabaya dhidi ya
mambo wasiyoyafahamu. Na katika mambo yale
wanayoyafahamu kwa hisia kama wanyama wa-
sio na akili, hayo ndiyo hasa yanayowaharibu.

11 Ole wao! Kwa kuwa wanaifuata njia ya
Kaini, wamekimbilia faida katika kosa la Bal-
aamu na kuangamia katika uasi wa Kora.

12 Watu hawa ni dosari katika karamu zenu za
upendo, wakila pamoja nanyi bila hofu, wakijil-
isha pasipo hofu. Wao ni mawingu yasiyokuwa
na maji, yakichukuliwa na upepo, miti isiyo
na matunda wakati wa mapukutiko, ambayo
hunyauka, iliyokufa mara mbili na kung’olewa
kabisa.
13 Wao ni mawimbi makali ya bahari, yakitoa
povu la aibu yao wenyewe, ni nyota zipoteazo,
ambao weusi wa giza ndio akiba waliowekewa
milele.

14 Enoki, mtu wa saba kuanzia Adamu alitoa
unabii kuhusu watu hawa, akisema: “Tazama,
Bwana anakuja pamoja na maelfu kwa maelfu
ya watakatifu wake,
15 ili kumhukumu kila mmoja na kuwapatiliza
wote wasiomcha Mungu kwa matendo yao yote
ya uasi waliyoyatenda, pamoja na maneno yote
ya kuchukiza ambayo wenye dhambi wamesema
dhidi yake.”
16 Watu hawa ni wenye kunung’unika na
wenye kutafuta makosa; wao hufuata tamaa zao
mbaya, hujisifu kwa maneno makuu kuhusu
wao wenyewe na kuwasifu mno watu wenye
vyeo kwa ajili ya kujipatia faida.

Maonyo Na Mausia

17 Lakini ninyi wapenzi, kumbukeni yale mi-
tume wa Bwana Yesu Kristo waliyonena zamani.
18 Kwa kuwa waliwaambia, “Siku za mwisho
kutakuwa na watu wenye kudhihaki, watakao-
fuata tamaa zao wenyewe za upotovu.”
19 Hawa ndio watu wanaowagawa ninyi, wa-
fuatao tamaa zao za asili, wala hawana Roho.
20 Lakini ninyi wapendwa, jijengeni katika
imani yenu iliyo takatifu sana tena ombeni
katika Roho Mtakatifu.
21 Jilindeni katika upendo wa Mungu mkitaza-
mia kwa furaha rehema ya Bwana wetu Yesu
Kristo ili awalete katika uzima wa milele.
22 Wahurumieni walio na mashaka;
23 wengine waokoeni kwa kuwanyakua ku-
toka kwenye moto; nao wengine wahurumieni
mkiwa na hofu, mkichukia hata vazi lenye
mawaa na kutiwa unajisi na mwili.

Dua Ya Kutakia Heri

24 Kwake yeye awezaye kuwalinda ninyi
msianguke na kuwaleta mbele za utukufu wake
mkuu bila dosari na kwa furaha ipitayo kiasi:
25 kwake yeye Mungu pekee Mwokozi wetu,
kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu, ukuu,
uweza na mamlaka ni vyake tangu milele, sasa
na hata milele! Amen.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™ (Bible)

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.
You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.
Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 1 Oct 2024 from source files dated 31 Aug 2023
9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462